



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**MWALIKO WA WATAZAMAJI WA UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE JIMBO  
LA DIMANI - ZANZIBAR NA UDIWANI KATIKA KATA 20 KWENYE  
HALMASHAURI MBALIMBALI TANZANIA BARA**

Kwa mujibu wa kifungu cha 46 (2) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 48 (2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kuendesha Uchaguzi Mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Dimani - Zanzibar na Udiwani katika Kata 20 kwenye Halmashauri mbalimbali Tanzania Bara, kujaza nafasi wazi kwenye Jimbo na Kata hizo zilizo wazi kutokana na sababu mbalimbali.

Kwa ajili ya kuweka uwazi katika Uchaguzi huo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuzingatia Kanuni ya 18 (2) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge 2015, inapenda kualika Asasi za Kiraia na Taasisi mbalimbali za ndani zinazotaka kuwa Watazamaji wa Uchaguzi katika Uchaguzi Mdogo unaotarajiwa kufanyika tarehe **22/01/2017**.

Ratiba ya Uchaguzi huo ni kama ifuatavyo:-

Na.	Tukio	Tarehe
1.	Kutoa Fomu za Uteuzi	10 - 22 Desemba, 2016
2.	Siku ya Uteuzi wa Wagombea	22 Desemba, 2016
3.	Kampani za Uchaguzi	23 Desemba, 2016 hadi 21 Januari, 2017
4.	Siku ya Kupiga Kura	22 Januari, 2017

Maeneo yatakayofanya Uchaguzi Mdogo ni:-

1. Jimbo la Dimani – Zanzibar,
2. Kata katika Halmashauri mbalimbali Tanzania Bara.

NA.	MKOA	NA.	HALMASHAURI	NA.	KATA
1.	Dodoma	1.	Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapa.	1	Ng'hambi
		2.	Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma.	2	Ihumwa
2.	Morogoro	3.	Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.	3	Kiwanja cha Ndege
3.	Iringa	4.	Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi.	4	Igombavanu
			Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi.	5	Ikweha
4.	Arusha	5.	Halmashauri ya Wilaya ya Meru.	6	Ngarenanyuki
5.	Dar Es Salaam	6.	Halmashauri ya Manispaa ya Temeke.	7	Kijichi
6.	Singida	7.	Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama.	8	Kinampundu
7.	Shinyanga	8.	Halmashauri ya Mji wa Kahama.	9	Isagehe
8.	Katavi	9.	Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe.	10	Kasansa
9.	Mwanza	10.	Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba.	11	Malya
		11.	Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema.	12	Kahumulo
10.	Ruvuma	12.	Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga.	13	Maguu
		13.	Halmashauri ya Manispaa ya Songea	14	Tanga
11.	Kagera	14.	Halmashauri ya Wilaya ya Muleba.	15	Kimwani
12.	Geita	15.	Halmashauri ya Wilaya ya Geita.	16	Nkome
13.	Kilimanjaro	16.	Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga.	17	Lembeni
14.	Manyara	17.	Halmashauri ya Wilaya ya Babati.	18	Duru

NA.	MKOA	NA.	HALMASHAURI	NA.	KATA
15.	Pwani	18.	Halmashauri ya Mji Kibaha.	19	Misugusugu
16.	Arusha	19.	Halmashauri ya Wilaya ya Arusha.	20	Mateves

Asasi/Taasisi zinapaswa kuzingatia masharti yafuatayo wakati wa kuwasilisha maombi yao.

- (i) Anuani Kamili ya Asasi inayotaka kutazama Uchaguzi,
- (ii) Mahali Asasi husika inapofanyia shughuli zake,
- (iii) Shughuli zinazofanywa na Asasi husika,
- (iv) Jimbo au Kata ambayo Asasi hiyo inataka kutazama Uchaguzi,
- (v) Idadi ya Watu itakaowatumia kutazama Uchaguzi, na
- (vi) Majina ya Viongozi wa Asasi husika kama yalivyoandikwa katika Nyaraka za Usajili wa Asasi/Taasisi hiyo.

Aidha, Asasi husika itatakiwa kuambatanisha nakala za nyaraka za uandikishaji/usajili wa Asasi hiyo.

Maombi ya kuwa Watazamaji wa Uchaguzi yatapaswa kuwasilishwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Makao Makuu kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi wa Uchaguzi,  
Tume ya Taifa ya Uchaguzi,  
Posta House, Ghorofa ya 7,  
Mtaa wa Ghana/Ohio,  
S. L. P. 10923,

**DAR ES SALAAM.**

Maombi yatatakiwa kuwasilishwa si zaidi ya tarehe 15 Januari, 2017.

